HOTUBA YA MHE. CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA UFUNGUZI WA KIKAO CHA WADAU WA ELIMU KWAAJILI YA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA ELIMU MKOA WA RUKWA TAREHE 31 JANUARI, 2024.

- ***Katibu Tawala wa Mkoa,***
- ***Mwenyekiti wa CCM Mkoa,***
- ***Wajumbe wa Kamati ya Usalama Mkoa,***
- ***Katibu wa CCM Mkoa,***
- ***Wahe. Wakuu wa Wilaya,***
- ***Makatibu Tawala Wasaidizi***
- ***Mstahiki Meya Manispaa ya Sumbawanga,***
- ***Wenyeviti wa Halmashauri,***
- ***Wakurugenzi wa Halmashauri,***
- ***Viongozi wa Madhehebu ya Dini,***
- ***Maafisa Elimu Msingi na Sekondari,***
- ***Viongozi wa Vyama vya Walimu,***
- ***Wathibiti Ubora wa Shule***
- ***Maafisa Elimu Kata,***
- ***Wakuu wa Shule, Walimu Wakuu na Walimu,***
- ***Wageni Waalikwa,***
- ***Wawakilishi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali,***
- ***Wadau wa Elimu,***
- ***Waandishi wa Habari,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ……..

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sisi kukutana mahali hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Kipekee sana niwatakie nyote **Heri ya Mwaka Mpya 2024**. Aidha namshukuru sana Katibu Tawala Mkoa kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika kikao hiki Muhimu katika sekta ya Elimu Mkoani kwetu. Pia niwape pole kwa safari ndefu walimu na

Viongozi kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wetu na ambao mmetenga Muda wenu kuhakikisha mnahudhuria katika kikao hiki Muhimu.

Ndugu Washiriki, Lengo kubwa la kikao hiki ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Elimu ndani ya Mkoa wetu kwa Mwaka 2023. Katika kikao hiki mtapata taarifa mbalimbali za shughuli za kielimu zinazohusu utekelezaji wa masuala ya kitaaluma na utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Shule na Halmashauri zetu. Mwisho tutakuwa na mijadala yenye lengo la kuboresha sekta hii muhimu.

Ndugu Washiriki, nipongeze jitihada kubwa zinazofanywa na walimu katika shule zetu zote za serikali na zisizo za serikali kuhakikisha ufaulu wa wanafunzi unaendelea kuimarika kwa mitihani ya kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita bila Kusahau Upimaji wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili. Ufafanuzi zaidi wa namna ambavyo tumetembea tutauona katika wasilisho litakalowasilishwa hivi punde katika kikao hiki.

Ndugu Washiriki, kama tulivyoona hadi tarehe 26 Januari 2024 Takwimu za Uandikishaji wa Wanafunzi wa darasa la Elimu ya Awali zinaonesha jumla ya wanafunzi **36,753** wameandikishwa na wameripoti sawa na asilimia **64.47** ya wote waliotarajiwa kuandikishwa. Wanafunzi **43,069** wameandikishwa na kuripoti sawa na **83.88** ya waliotarajiwa. Wanafunzi **15,684** wa Kidato cha Kwanza wameripoti kati ya wanafunzi **24,409** waliochaguliwa. Natoa pongezi kwa mafanikio hayo ya uandikishaji, hata hivyo niwatake kuhakikisha kuwa hakuna mtoto atayebaki nyumbani mwenye umri wa kuandikishwa shule wakiwemo wenye mahitaji maalum, wote waripoti shuleni. Viongozi wa ngazi zote wawajibike kuhakikisha Watoto wote wanaandikishwa shule.

Ndugu Washiriki, Kati ya wanafunzi **24,415** waliofaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na kuwa na sifa za kujiunga na sekondari za kutwa tumeweza kuwachagua wote kujiunga na shule zetu za sekondari za Kata Mkoani kwetu. Aidha, wanafunzi **139** wamechaguliwa kujiunga na shule za bweni na vipaji maalumu nje ya Mkoa. Tunamshukuru sana Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wetu kwa kuhakikisha kuwa Watoto wote wanachaguliwa kwa kuleta fedha za kujenga Miundombinu.

Ndugu Washiriki, Niishukuru sana serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kutusaidia kuongeza Miundombinu mbalimbali ya shule za Msingi na Sekondari kwa mwaka 2023 – 2024 ikiwemo ujenzi wa Shule Mpya za Msingi na Sekondari. Shule mpya za Sekondari za Kata zilizopata usajili na kupangiwa wanafunzi mwezi huu wa Januari, 2024 hii ni Jumla ya Shule Nne (4) ambazo ni **Shule ya Sekondari Josephat Kandege** Katika Kata Ya Mpombwe Wilaya ya Kalambo, **Shule za Sekondari Kapita** Kata ya Ninde na **Shule ya Sekondari Ntatumbila** Kata ya Ntatumbila Wilaya ya Nkasi, **Shule ya Sekondari Mazoezi** iliyoko Kata ya Chanji Wilaya ya Sumbawanga (Manispaa). Aidha, ndani ya mwaka huu shule Mpya mbili za sekondari zinatarajiwa kukamilika na kuanza kusajili wanafunzi, hii ni shule ya sekondari ya wasichana ya Mkoa na shule ya Sekondari katika kata ya Kalumbaleza zote katika Halmashauri ya wilaya ya sumbawanga.

Ndugu Washiriki, Kwa upande wa Shule za Msingi, Shule mpya zilizoongezeka na kupata usajili kamili katika Halmashauri zetu ni Shule ya Msingi KALEPULA B, na NAMLANGWA za Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Shule ya Msingi KITUKU na MUUNGANO za Halmashauri ya Wilaya NKASI, Shule ya Msingi LANCHI na TUWI za Halmashauri ya Wilaya ya SUMBAWANGA, na Shule ya Msingi MPASI na SOKOLO za Halmashauri ya Manispaa ya SUMBAWANGA. Naomba nisisitize utunzaji wa Miundombinu yote iliyojengwa pamoja na kupanda miti ya Kivuli na Matunda katika Shule zote Za Msingi na Sekondari za Mkoa wetu.

Ndugu Washiriki, Naomba nipongeze shule zote zilizofanya vizuri katika Mitihani mwaka 2023. Aidha, niwapongeze sana walimu ambao kwa siku ya leo mtatunukiwa vyeti vya kutambua umahiri na mchango wenu katika Ufaulu wa Masomo ambayo mmefundisha watahiniwa wetu mwaka 2023. Nipende kusema kwamba mmekuwa sehemu ya walimu ambao mtatumika katika shughuli za kielimu hasa katika kazi maalumu za kitaaluma ndani ya Mkoa wetu. Hivyo, ongezeni bidii zaidi katika maeneo yenu ili muwe mfano wa kuigwa.

Ndugu Washiriki, Ndugu Washiriki, kabla ya kumalizia hotuba yangu naagiza na kusisitiza mambo yafuatayo:-

1. Usimamizi na Ukamilishaji wa miradi:

Niwatake Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa shule na Kamati za Usimamizi wa Miradi kuhakikisha kwamba Miradi yote ambayo haijakamilika, ikamilishwe ili iweze kutumiwa na wanafunzi haraka iwezekanavyo. Aidha, kwa miradi yote itakayokuja kuanzia sasa tuhakikishe inaanza mara moja na ikamilike kwa kuwa fedha sio kikwazo. Viongozi wa Siasa, Halmashauri na Wilaya tusiingilie michakato ya Ujenzi kuanzia kutafuta mafundi na wazabuni wa vifaa, suala zima liachiwe kamati za ujenzi. Aidha Miongozo ya serikali kuhusu ujenzi izingatiwe.

2. Usimamizi wa Taaluma na Maendeleo ya Shule

Niwatake Vingozi wa Elimu ngazi ya Mkoa, Wilaya na Shule. Jitihada zinahitajika kuongeza ufaulu katika Upimaji kwa Darasa la Nne na Kidato cha Pili. Mkoa unahitaji kuona tunapata ufaulu wa asilimia **100** katika Mitihani yote. Katika ngazi zote hizo za Usimamizi Elimu kwa kuweka malengo katika utekelezaji wa majukumu yenu kuanzia mwalimu wa somo. Aidha, katika Taasisi zenu muwe kitu kimoja katika kupanga na kutekeleza malengo. Tushirikiane kwa umoja wetu tutapiga hatua kubwa sana katika maendeleo ya elimu ya Mkoa wa Rukwa. Tunajua kuna changamoto mbalimbali ambazo walimu wanazo, serikali itaendelea kuzipokea na kuzitatua siku hadi siku.

3. Kukuza Ubunifu na Kufanya Kazi kwa bidii.

Lengo kubwa la Kuboresha Mitaala ya Elimu ni kuhakikisha Ubora wa Elimu uliokusudiwa unafikiwa, niwatake wasimamizi wa Elimu ngazi zote kuhakikisha mnakuza ubunifu utakaochochea mabadiliko chanya kwa walimu na wanafunzi wanaowasimamia. Aidha, kila mwalimu afanye kazi kwa bidii na kuongeza ubunifu katika ufundishaji na ujifunzaji. Niwatake walimu kujibidiisha katika kuongeza ujuzi na umahiri kupitia mafunzo kazini ngazi ya shule, kata na Wilaya. Nizitake Halmashauri kuhakikisha wanasimamia eneo hili ili tupate mabadiliko chanya tunayohitaji.

4. Kusikiliza na Kutatua kero za Walimu

Niwatake Wakurugenzi, Maafisa Elimu na Wasimamizi wa Elimu ngazi mbalimbali kuwasikiliza walimu na kujitahidi kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili ambazo utatuzi wake upo katika ngazi zenu. Itakuwa jambo la Kusikitisha iwapo kero ya mwalimu ambayo Mkuu wa shule anaweza kuimaliza kituoni ikawa ni lalamiko ambalo linapitiliza hadi

ngazi ya Mkoa. Tukitatua changamoto hizi tukianzia sehemu za kazi tutapiga hatua na walimu watatulia katika vituo vyao wakifanya kazi.

5. Kutoa huduma ya chakula cha Mchana shuleni

Ndugu wajumbe, niwatake Wakuu wa Wilaya, wakurugenzi wa Halmashauri wakishirikiana na wenyeviti, Watendaji wa Kata, Kamati na Bodi za Shule kuhakikisha kuwa utoaji wa chakula kwa wanafunzi unafikia asilimia 100 kwa shule zetu za Msingi na Sekondari. Suala hili liende sambamba na Kupunguza Utoro shuleni.

Ndugu washiriki, niwashukuru sana kwa kuhudhuria kikao hiki Muhimu; niwatakie mjadala mwema utakaoleta chachu katika maendeleo ya elimu Mkoani kwetu na nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yenu.

Mungu Ibariki Tanzania,
Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa
Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Charles Makongoro Nyerere
Mkuu wa Mkoa wa Rukwa